Jamhuri ya
Muungano wa
Tanzania

Wizara ya Fedha

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA 2024

## Toleo la Mwananchi



# HALI YA UCHUMI WA TAIFA 2024

**Toleo la Mwananchi**

Wizara ya Fedha
Mji wa Serikali- MTUMBA
Mtaa wa Hazina, 40468 Dodoma



> Serikali imekuwa ikitekeleza miradi katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo sekta za uzalishaji, miundombinu na huduma za kijamii kwa lengo la kujenga uchumi shindani kwa maendeleo ya watu. Aidha, Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejipambanua vyema katika kutekeleza miradi yenye matokeo chanya katika sekta mbalimbali hususan zile ambazo zinagusa maisha ya wananchi moja kwa moja, kwa kuongeza ajira hususan kwa vijana, kuongeza mapato ya Serikali na kukuza uchumi shirikishi.

Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba
**Waziri wa Fedha**

Wizara ya Fedha

Idara ya Uchambuzi wa Sera



"Taarifa ya Hali ya Uchumi Toleo la Mwananchi inaelezea mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi na kijamii kwa mwaka 2024. Taarifa hii inatoa maelezo ya ufanisi wa sekta mbalimbali kwa njia ambayo ni rahisi kueleweka kwa jamii yote kwa ujumla."

Dkt. Natu E. Mwamba,
**Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha**

Wizara ya Fedha

Idara ya Uchambuzi wa Sera

# YALIYOMO

## 01

## Uchumi Jumla

### Ukuaji wa Uchumi


- Uchumi wa Dunia 1
- Mfumuko wa Bei wa Dunia 3
- Uchumi waTaifa 5
- Mfumuko wa Bei wa Taifa 7


### Sekta ya Fedha


- Mikopo sekta Binafsi 8
- Viwango vya Riba, Thamani ya Shilingi 8


### Sekta ya Nje


- Biashara ya Bidhaa na Huduma, 9
- Urari wa Malipo, 10
- Akiba ya Fedha ya Kigeni 10


### Idadi ya Watu


- Idadi ya Watu 11
- Idadi ya Watu kimkoa 11
- Idadi ya Watu kwa Jinsi na Umri 12
- Nguvu kazi na Ajira 12


## 02

## Fedha za Serikali


- Mapato ya Serikali 13
- Matumizi ya Serikali 14




## 03

## Sekta za Uzalishaji

### Kilimo


- Mazao, 15
- Upatikanaji wa Pembejeo 16 17
- Ufugaji 17
- Uvuvi 17


### Viwanda


- Uzalishaji wa Bidhaa, 19
- Usajili, Ushindani na Udhibiti wa bidhaa bandia 20


### Madini


- Leseni za Shughuli za Madini 21
- Vibali 22


### Nishati


- Uzalishaji wa Umeme 23
- Gesi Asilia 24
- Bei za Mafuta 24

# 04

## Miundombinu

### Mawasiliano


- Mawasiliano 25
- Habari 26
- Sanaa 26
- Michezo 26


### Ujenzi


- Usajili wa Barabara 27
- Usajili wa Makandarasi 28
- Wahandisi 28


### Uchukuzi


- Usafiri 15
- Abiria 16
- Shehena zilizohudumiwa 31


# 05

## Huduma za Jamii

### Elimu


- Elimu ya Msingi 32
- Elimu ya Sekondari 33
- Elimu ya Ufundi Stadi-VETA 34
- Elimu ya Juu 35


### Afya


- Vituo vya Kutolea Huduma za Afya 36
- Udhibiti wa Kifua Kikuu na Malaria 38
- Afya kwa Watoto 38


### Maji


- Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji 39
- Upatikanaji wa Maji 40
- Uondoaji wa Majtaka 40


# 06

## Sekta Nyingine

### Utalii


- Mwenendo wa Utalii 41
- Hifadhi za Taifa 42


### Sekta Binafsi


- Usajili wa Miradi ya Uwekezaji 43
- Uwekezaji wa Sekta Binafsi kutoka Nje 43


### Masuala mtambuka


- Mazingira 45
- Usalama wa Raia, pamoja na Usajili 45
- Ufilisi na Udhamini 45


# 07

## Suala Maalumu

### Uendelezaji Wa Nishati Safi Ya Kupikia


- Utangulizi 47
- Hali Ilivyo 48
- Athari za Matumizi ya Nishati Isiyo Safi ya Kupikia 49
- Changamoto Zinazo-athiri Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 50
- Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto Zilizopo 51
- Sekta Binafsi 51




# VIELELEZO


Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Duniani Mwaka 2024 (Asilimia) 1
Kielelezo Na. 1.2: Wastani wa Ukuaji wa Uchumi wa Kikanda (Asilimia) 2
Kielelezo Na. 1.3: Wastani wa Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Asilimia) 4
Kielelezo Na.1.4: Ukuaji wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi Mwaka 2023-2024 (Asilimia) 5
Kielelezo Na. 1.5: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Mwaka 2021-2024 (Asilimia) 5
Kielelezo Na.1.6: Mchango wa Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa Mwaka 2024 (Asilimia) 6
Kielelezo Na.1.7: Mchango wa Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa Mwaka 2024 (Asilimia) 6
Kielelezo Na. 1.8. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Baadhi ya Makundi 7
Kielelezo Na.2.1: Mchango wa Mikopo iliyotolewa na Benki za Biashara kwa Shughuli za kiuchumi, Mwaka 2023-2024 (Asilimia) 8
Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa, Mwaka 2021-2024 9
Kielelezo Na. 3.2: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa Nje, Mwaka 2024 9
Kielelezo Na. 3.3: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa Zisizo Asilia Zilizouzwa Nje Mwaka 2024 10
Kielelezo Na.3.4: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa zilizoagizwa kutoka Nje Mwaka 2024 10
Kielelezo Na. 3.5: Mwenendo wa Biashara ya Huduma, Mwaka 2021-2024 10
Kielelezo Na. 4.1: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsia Mwaka 2024 12
Kielelezo Na. 4.2: Mchango wa Mkoa katika Ajira Rasmi kwa Mwaka 2022/23 12
Kielelezo Na. 5.1: Mchanganuo wa Mapato ya Ndani kwa Kipindi cha Julai 2024-Machi 2025 13
Kielelezo Na. 5.2: Mchanganuo wa Misaada na Mikopo , Julai 2024-Machi 2025 13
Kielelezo Na. 5.3: Mchanganuo wa Ridhaa ya Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2024-Machi 2025 14
Kielelezo Na. 6.1: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Chakula Mwaka 2021-2024 15
Kielelezo Na. 6.2: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Biashara Mwaka 2021-2024 16
Kielelezo Na.6.3: Mwenendo wa Uzalishaji na Matumizi ya Mbolea Mwaka 2020/21-2023/24 16
Kielelezo Na. 6.4: Mwenendo wa Idadi ya Mifugo Mwaka 2023 - 2024 17
Kielelezo Na. 6.5: Uzalishaji wa Nyama Mwaka 2023-2024 17
Kielelezo Na. 6.6: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mayai 17
Kielelezo Na. 6.7: Mwenendo wa Uvunaji wa Samaki 2021 - 2024 17
Kielelezo Na. 6.8: Mchanganuo wa Aina ya Uvunaji Samaki kwa Mwaka 2023 18
Kielelezo Na. 7.1: Ukuaji wa Uzalishaji wa Baadhi ya Bidhaa za Viwandani Mwaka 2024 19
Kielelezo Na. 7.2: Uzalishaji wa Saruji, Mwaka 2020-2024 19
Kielelezo Na. 8.1: Mwenendo wa Uzalishaji na Kiasi cha Dhahabu Kilichopata Vibali vya Kuuzwa Nje, Mwaka 2021 - 2024 22
Kielelezo Na 9.1: Ukuaji wa Uwezo wa Uzalishaji wa Umeme, Mwaka 2020-2024 23
Kielelezo Na. 9.2: Mchanganuo wa Umeme Uliozalishwa Mwaka 2024 23

Kielelezo Na. 9.3: Mwenendo wa Mchango wa Umeme uliozalishwa katika Gridi ya Taifa, Mwaka 2021-2024 23
Kielelezo Na. 9.4: Umeme Uliouzwa kwa Watumiaji Mbalimbali, Mwaka 2020-2024 24
Kielelezo Na. 9.5: Mwenendo wa Uzalishaji wa Gesi Asilia, Mwaka 2020-2024 24
Kielelezo Na. 9.6: Mwenendo wa Bei ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa katika Soko la Ndani Mwaka 2024 (Shilingi/Lita) 24
Kielelezo Na. 10.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Gharama za Kupiga Simu kwa Dakika, Mwaka 2021-2024 25
Kielelezo Na. 10.2: Mchanganuo wa Usajili wa Vyombo vya Habari, Mwaka 2021 - 2024 26
Kielelezo Na. 10.3: Mchanganuo wa Wasanii Binafsi Waliosajiliwa Mwaka 2024) 26
Kielelezo Na. 10.4: Mwenendo wa Idadi Usajili wa Vilabu vya Michezo, Mwaka 2021-2024 26
Kielelezo Na.11.1: Usimamizi wa Mtandao wa Barabara 27
Kielelezo Na. 11.2: Hali ya Mtandao wa barabara Kuu na za Mikoa 28
Kielelezo Na.11.3: Mchanganuo wa Wahandisi waliosajiliwa na Bodi ya Wahandisi kwa mwaka 2024 28
Kielelezo Na. 12.1: Mwenendo wa Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, Mwaka 2021-2024 29
Kielelezo Na. 12.2: Mchanganuo wa Ajali Mwaka 2024 29
Kielelezo Na. 12.3: Mwenendo wa Ajali za Barabarani, Mwaka 2020-2024 30
Kielelezo Na. 12.4: Mchanganuo wa Abiria Mwaka 2024 30
Kielelezo Na. 12.5: Mchanganuo wa Shehena Zilizohudumiwa kwa Bandari Mwaka 2024 31
Kielelezo Na. 13.1: Mwenendo wa Idadi ya Shule za Msingi Mwaka 32
Kielelezo Na. 13.2: Mwenendo wa Idadi Shule za Msingi za Serikali na Zisizo za Serikali, Mwaka 2021-2024 33
Kielelezo Na. 13.3: Mgawanyo wa Wanafunzi kwa Jinsi katika Shule za Msingi Mwaka 2024 33
Kielelezo Na. 13.4: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na waliofaulu Darasa la Saba, Mwaka 2020-2024 33
Kielelezo Na. 13.5: Mwenendo wa Idadi ya Shule za Sekondari, Mwaka 2021-2024 33
Kielelezo Na. 13.6: Mwenendo wa Idadi ya Shule za Sekondari za Serikali na Zisizo za Serikali, Mwaka 2021-2024 33
Kielelezo Na. 13.7: Mwenendo wa Idadi ya Wanafunzi Kidato cha I-VI, Mwaka 2021-2024 34
Kielelezo Na. 13.8: Mgawanyo wa Wanafunzi kwa Jinsia Katika Shule za Sekondari Kidato cha I-VI Mwaka 2024 34
Kielelezo Na. 13.9: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na Ufaulu Kidato cha Nne, Mwaka 2021-2024 34
Kielelezo Na. 13.10: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na Ufaulu Kidato cha Sita, Mwaka 2021-2024 34
Kielelezo Na. 13.11. Mwenendo wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu 35
Kielelezo Na. 13.12. Mchanganuo wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa Jinsia Mwaka 2023/24 35
Kielelezo Na. 13.13: Mwenendo wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Wanufaika wa Mkopo Mwaka 2020/21-20023/24 35
Kielelezo Na. 14.1: Mchanganuo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya kwa Umiliki Mwaka 2024 36
Kielelezo Na. 14.2: Mwenendo wa Idadi ya Wagonjwa Waliohudumiwa Mwaka 2021-2024 37
Kielelezo Na. 14.3: Idadi ya Wagonjwa wa Nje katika Vituo vya vya kutolea Huduma za Afya, Mwaka 2021-2024 37
Kielelezo Na. 14.4: Idadi ya Wagonjwa Waliolazwa katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya, Mwaka 2021-2024 37
Kielelezo Na. 14.5: Mwenendo wa Ununuzi wa Dawa, Vyandarua na Vitendanishi, Mwaka 2023-2024 38
Kielelezo Na. 14.6: Watoto wa Chini ya Mwaka Mmoja Waliopata Chanjo Mwaka 2024 38
Kielelezo Na. 15.1: Mwenendo wa Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji Mijini na Vijijini, Mwaka 2021-2024 40
Kielelezo Na. 15.2: Wateja walioonganishwa na mtandao wa majitaka, Mwaka 2021-2024 40
Kielelezo Na. 15.3: Mtandao wa majitaka, Mwaka 2021-2024 40
Kielelezo Na. 16.1: Mwenendo wa Biashara ya Utalii Nchini, Mwaka 2021-2024 41
Kielelezo Na. 16.2: Mchanganuo wa Watalii Waliongia Nchini kwa Maeneo Waliotembelea Mwaka 2024 41
Kielelezo Na. 16.3: Mchanganuo wa Watalii waliotembelea Hifadhi za Taifa 2024 42
Kielelezo Na. 17.1: Mchanganuo wa Miradi iliyosajiliwa Mwaka 2024 43
Kielelezo Na. 17.2: Mchanganuo wa Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje ya Nchi Mwaka 2023 44
Kielelezo Na. 18.1: Mchanganuo wa Makosa Makubwa ya Jinai Mwaka 2024 45
Kielelezo Na. 18.2: Mwenendo wa Hati za Viapo vya Ndoa na Hati za Talaka, Mwaka 2021-2024 45
Kielelezo Na. 18.3: Idadi ya Usajili wa Hati Mbalimbali chini ya Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA kwa Mwaka 2024 46
Kielelezo Na. 19.1: Uzalishaji wa Hewa Ukaa Kikanda 48
Kielelezo Na. 19.2:Uzalishaji wa Hewa Ukaa katika Ngazi ya Nchi Mwaka 2000 na 2023 48
Kielelezo Na. 19.3: Upatikanaji wa Nishati Safi na Teknolojia ya Kupikia Kikanda Mwaka 2000 na 2022 (Asilimia) 48
Kielelezo Na. 19.4: Mwenendo wa Matumizi ya Nishati Safi na Teknolojia ya Kupikia Tanzania Mwaka 2010 – 2022 48
Kielelezo Na. 19.5: Matumizi ya Nishati ya Kupikia kwa Kaya, 2019/20 49
ielelezo Na. 19.6: Matumizi ya Kuni Kama Nishati ya Kupikia katika Ngazi ya Mkoa, Mwaka 2017/18 (Asilimia ya Kaya) 49
Kielelezo Na. 19.7: Matumizi ya Mkaa Kama Nishati ya Kupikia katika Ngazi ya Mkoa Mwaka 2017/18 (Asilimia ya Kaya) 49
Kielelezo Na. 19.8: Mwenendo wa Matumizi wa Nishati ya Kuni na Mkaa Mwaka 2007 – 2017/18 (Asilimia ya Kaya) 49



# 1

# Uchumi Jumla



Ukuaji wa Uchumi
Sekta ya Fedha
Sekta ya Nje
Idadi ya Watu

# UKUAJI WA UCHUMI

## Uchumi wa Dunia, Mfumuko wa Bei wa Dunia, Uchumi waTaifa Mfumuko wa Bei wa Taifa



### Uchumi wa Dunia



**3.3%**

Ukuaji wa Uchumi wa dunia katika mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kulichangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo: athari za utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika kukabiliana na mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea; migogoro ya kisiasa hususan Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati; gharama kubwa za mikopo katika masoko ya fedha zilizoathiri zaidi nchi zinazoendelea; na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Duniani Mwaka 2024**



**Kielelezo Na 1.2: Wastani wa Ukuaji wa Uchumi wa Kikanda (Asilimia)**






## Mfumuko wa Bei wa Dunia



**5.8%**

Kiwango cha mfumuko wa bei wa dunia kwa mwaka 2024 ambacho kimepungua ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kuimarika kwa bei za bidhaa na huduma duniani kulitokana na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kupunguza ongezeko la ukwasi, kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan mafuta na mbolea.





**2.6%**

Kiwango cha Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023.



**16.8%**

Kiwango cha mfumuko wa bei kwa kwa nchi zinazoibukia na zinazoendelea za Ulaya ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.1 mwaka 2023.

**Mfumuko wa Bei Kusini mwa Jangwa la Sahara**

Mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa wastani wa asilimia 18.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.6 mwaka 2023. Ongezeko la mfumuko wa bei lilichangiwa na athari za kushuka kwa thamani ya fedha pamoja na kushuka kwa uzalishaji katika shughuli za kilimo kwa baadhi ya nchi.

**Kielelezo Na 1.3: Wastani wa Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Asilimia)**



## Uchumi wa Taifa

**5.5%**

Ukuaji wa Pato halisi la Taifa mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.1 katika mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 1.5: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Mwaka 2021-2024 (Asilimia)**




**17.1%**

Shughuli za sanaa na burudani iliendelea kuongoza kwa kuwa na ukuaji mkubwa kuliko shughuli nyingine nyingine.



**Ukuaji huo ulichangiwa na:**

- Utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji;
- Kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere;
- Hali nzuri ya hewa iliyoimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo.
- Usafirishaji wa abiria kupitia Reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa – SGR kwa kipande cha kutoka Dar es salaam hadi Dodoma;
- Kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; na

**Kielelezo Na.1.4: Ukuaji wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi Mwaka 2023-2024 (Asilimia)**




Shughuli za ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ilifuatia kwa kuwa na asilimia 14.4, habari na mawasiliano asilimia 14.3 na shughuli ya fedha na bima asilimia 13.





**Kielelezo Na.1.6: Mchango wa Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa Mwaka 2024 (Asilimia)**






**26.3%**

Shughuli za kilimo ziliendelea kuongoza kwa kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ikifuatiwa na ujenzi asilimia 12.8 na uchimbaji madini na mawe asilimia 10.1.

Pamoja na shughuli za sanaa kuwa na ukuaji mkubwa bado imeendelea kuwa na mchango mdogo katika uchumi pamoja na katika ukuaj wa uchumi.



Kwa upande mwingine, shughuli za kilimo, ujenzi, fedha na bima, uchimbaji madini na mawe, na biashara na matengenezo ziliendelea kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa. Katika kipindi hicho, shughuli hizo zilichangia zaidi ya asilimia 50 ya ukuaji wa Pato la Taifa.

**Kielelezo Na.1.7: Mchango wa Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa Mwaka 2024 (Asilimia)**



## Mfumuko wa Bei wa Taifa





**9.3%**

**Mfumuko wa bei kwa kundi la nishati, mafuta na ankara za maji kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2023.**

**3.1%**

Kiwango cha mfumuko wa Bei kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulipungua kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani.

**Kielelezo Na. 1.8. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Baadhi ya Makundi**






**3.4%**

Kiwango cha wastani wa mfumuko wa bei za msingi kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2023.



**2.1%**

Kiwango cha mfumuko bei wa kwa kundi la chakula na vinywaji baridi kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kufuatia uwepo wa hali nzuri ya hewa na utolewaji wa ruzuku ya mbolea pamoja na kuimarishwa kwa miundombinu ya umwagiliaji na usafirishaji.



# SEKTA YA FEDHA

## Mikopo sekta Binafsi, Viwango vya Riba, Thamani ya Shilingi




### Mikopo kwa Sekta Binafsi

**12.4%**

Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi na kufikia shilingi bilioni 36,097.4 mwaka 2024, ikilinganishwa na shilingi bilioni 32,102.0 mwaka 2023.

**Kielelezo Na.2.1: Mchango wa Mikopo iliyotolewa na Benki za Biashara katika baadhi ya Shughuli za kiuchumi Mwaka 2023-2024 (Asilimia)**




### Viwango vya Riba

**9.17%**

Wastani wa riba za amana za mwaka mmoja mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 8.65 mwaka 2023.



**15.82%**

Wastani wa riba za mikopo ya mwaka mmoja mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 16.53 mwaka 2023.

### Thamani ya Shilingi na Ujazi wa Fedha

**9.0%**

Kasi ya kushuka kwa thamani ya shilingi katika mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023.

**9.2%**

Ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2 ) mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 11.9 mwaka 2023.



# SEKTA YA NJE

## Biashara ya Bidhaa na Huduma, Urari wa Malipo, Akiba ya Fedha ya Kigeni



### Biashara ya Bidhaa

**18.5%**

Kasi ya ongezeko la thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kufikia dola za Marekani 9,121.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola milioni 7,696.6 mwaka 2023.



**Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa, Mwaka 2021-2024**




**4.0%**

Ongezeko la uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kufikia dola za Marekani milioni 14,278.9 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola milioni 13,728.9 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji.

**Kielelezo Na. 3.2: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa Nje, Mwaka 2024**



**Kielelezo Na. 3.3: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa Zisizo Asilia Zilizouzwa Nje Mwaka 2024**




**Kielelezo Na.3.4: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa zilizoagizwa kutoka Nje Mwaka 2024**






## Biashara ya Huduma




# 4,290.5

Dola za Marekani milioni

Ziada ya urari wa biashara ya huduma mwaka 2024 sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 11.9. Hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii kutokana na kuimarika kwa sekta hiyo pamoja na kuongezeka kwa mapato ya huduma za usafirishaji.

**Kielelezo Na. 3.5: Mwenendo wa Biashara ya Huduma, Mwaka 2021-2024**




## Mizania ya Malipo na Nchi za Nje

### Urari wa Malipo yote

# 80.5

Dola za Marekani milioni

Ziada ya urari wa malipo yote ya nje kwa mwaka 2024, ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 41.9 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa ziada ya urari wa mapato yatokanayo na huduma.

### Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma

# -866.7

Dola za Marekani milioni

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa na huduma kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,196.5 mwaka 2023. Kupungua kwa nakisi kulitoka-na na kuimarika kwa urari wa biashara ya huduma.

### Akiba ya Fedha za Kigeni

# 5,546.9

Dola za Marekani milioni



Kiasi kilichotosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi 128 hadi Desemba 2024 kwa kipindi cha miezi 4.4.

# RASILIMALI WATU

## Idadi ya Watu, Idadi ya Watu kimkoa, Idadi ya Watu kwa Jinsi na Umri, Nguvu kazi na Ajira



### Idadi ya Watu



**4.1%**

Ongezeko la mwaka la makadirio ya idadi ya watu Tanzania kwa mwaka 2024 na kufikia 66,278,276. Aidha, wanawake walikadiriwa kuwa 33,799,398, sawa na asilimia 51 ya watu wote na wanaume wali-kuwa 32,478,878 (asilimia 49) .Makadirio ya mwaka 2024 ni maoteo ya mwenendo wa matokeo ya Sensa ya Mwaka 2022 kwa kutumia mbinu ya kipeo.

Makadirio ya Idadi ya watu kwa Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na mchango wake katika asilimia ya makadirio ya Jumla idadi ya watu Tanzania.






### Idadi ya Watu Kimkoa

**8.9%**

Mchango wa Idadi ya watu Dar esalam kwa jumla ya idadi ya watu Tanzania Bara.



Mwaka 2024, mkoa wa Dar es Salaam uliku-wa na idadi kubwa zaidi ya watu wapatao 5,739,734,ikifuatiwa na mkoa wa Mwanza uliokuwa na watu 3,992,565.

Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam ilichangiwa na upatikanaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi zilizowavutia watu kuhamia kutoka mikoa mingine na urahisi wa upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii.



**47.2%**

Mchango wa mkoa wa Mjini Magharibi kwa jumla ya watu wote Tanzania Zanzibar.



**15%**

Mkoa wa Njombe ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu, wapatao 939,503, sawa na asilimia 1.5 ya watu wote Tanzania Bara

## Idadi ya watu kwa jinsi na Umri Tanzania



**53.0%**

Asilimia ya Kundi la umri wa miaka 15-64 (nguvu kazi) liliongoza kuwa na mchango kumbwa katika idadi ya watu

**Kielelezo Na. 4.1: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsia Mwaka 2024**




Idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 35 imekua ya pili kwa idadi ya watu, kwa kuchangia asilimia 34.1 ya watu wote.



Watu wenye umri tegemezi ambao ni umri chini ya miaka 15 na umri wa miaka 65 na zaidi walikuwa 30,195,205, sawa na asilimia 47.0 ya watu wote.

## Nguvu Kazi na Ajira



**3,635,755**

Jumla ya ajira rasmi kwa mujibu wa Utafiti wa Ajira na Mapato katika sekta rasmi kwa mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 5.4 ikilinganishwa na 2019/20

**Kielelezo Na. 4.2: Mchango wa Mkoa katika Ajira Rasmi kwa Mwaka 2022/23**




**33.2%**

Dar es salaam uliongoza kwa kuchangia asilimia kubwa ya waajiriwa wote kwa mwaka 2022/23, ikifuatiwa na morogoro iloyochangia 8.0.

**< 1%**

Kiwango cha chini zaidi cha ajira kwa mujibu wa tafiti kwa mkoa. Ajira hizi ziliтоlewa na mkoa wa Songwe na Katavi




# 2

# Fedha za Serikali



Mapato ya Serikali
Matumizi ya Serikali

# FEDHA ZA SERIKALI

## Mapato ya Serikali, Matumizi ya Serikali



### Mapato ya Serikali

**100.2%**

Ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho.



**Kielelezo Na. 5.1: Mchanganuo wa Mapato ya Ndani kwa Kipindi cha Julai 2024-Machi 2025**




**Kielelezo Na. 5.2: Mchanganuo wa Misaada na Mikopo , Julai 2024-Machi 2025**




[1]Mapato haya ni jumla ya mapato ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Mamlaka ya Serikali za Mitaa

## Mwenendo wa Matumizi



**Ridhaa ya matumizi ya ya maendeleo iliyotolewa ilijumuisha ugharamiaji wa miradi ya miundombinu wezeshi na huduma za jamii**

**91.4%**

Ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho.

**Kielelezo Na. 5.3: Mchanganuo wa Ridhaa ya Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2024-Machi 2025**



# 3

# Sekta za Uzalishaji




Kilimo
Viwanda
Madini
Nishati

# KILIMO

## Mazao, Upatikanaji wa Pembejeo, Ufugaji, Uvuvi



### Mazao

**Mazao ya Chakula**

**128%**

Kiwango cha utoshelevu wa chakula cha nchi kulingana na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2024.



**11.8%**

Ongezeko la uzalishaji wa mazao makuu ya chakula Mwaka 2024 na kufikia tani 22,803,316 kilinganishwa na uzalishaji wa mwaka 2023

**Kielelezo Na. 6.1. Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Chakula Mwaka 2021-2024**




**Mazao ya Biashara**

**22.1%**

Ongezeko la uzalishaji wa mazao asilia ya biashara na kufikia tani 1,487,3643 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 1,218,136[2] mwaka 2023. Hii linatokana na wakulima kuendelea kufuata kanuni bora za kilimo cha mazao ya biashara.



**Kielelezo Na. 6.2. Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Biashara Mwaka 2021-2024**




[2]Takwimu ya mwaka 2023 imebadilika kutokana na mapitio ya mazao ya pamba,pareto, chai, korosho na mkonge



Upungufu wa mazao ya bustani ulitokana na uwepo wa mvua nyingi na visumbufu vilivyosababisha upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna.



## Mazao ya Bustani

**-11.5%**

Upungufu wa uzalishaji wa mazao ya bustani unaojumuisha maua, matunda, viungo na mboga na kufikia tani 7,513,501.7 mwaka 2024 ikilganishwa na uzalishaji mwaka 2023.

## Upatikanaji wa Pembejeo

### Mbegu Bora

**22.5%**

Ongezeko la upatikanaji wa mbegu bora na kufikia tani 72,031.89 Mwaka 2024 ikilinganishwa na upatikanaji wa mbegu bora mwaka 2023.

### Mbolea

**17.5%**

Ongezeko la upatikanaji wa mbegu bora na kufikia tani 72,031.89 Mwaka 2024 ikilinganishwa na upatikanaji wa mbegu bora mwaka 2023. Aidha, uzalishaji wa ndani ulikuwa tani 158,628 ikilinganishwa na tani 84,696 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 87.3. Uzalishaji huo ni sawa na uwiano wa asilimia 14.6 wa kiasi kilichotumika ndani ya nchi.

**Kielelezo Na.6.3. Mwenendo wa Uzalishaji na Matumizi ya Mbolea Mwaka 2020/21-2023/24**




## Ufugaji

### Uzalishaji wa Mifugo

**3.4%**

Ongezeko la ukuaji wa idadi ya ng'ombe nchini na kufikia kuwa ng'ombe milioni 39.2 ikilinganishwa na ng'ombe milioni 37.9 mwaka 2023.



**Kielelezo Na. 6.4. Mwenendo wa Idadi ya Mifugo Mwaka 2023 - 2024**




### Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo

**20.0%**

Ongezeko la uzalishaji wa nyama mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 803,264.3 mwaka 2023. Aidha, mayai milioni 6,409.2 yalizalishwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mayai milioni 5,500 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 16.5. Vilevile, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kwa asilimia 10.3 na kufikia lita milioni 3,971.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na lita milioni 3,600 zilizozalishwa mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 6.5. Uzalishaji wa Nyama Mwaka 2023-2024**




**Kielelezo Na. 6.6. Mwenendo wa Uzalishaji wa Mayai**




## Uvuvi

### Uvunaji wa Samaki

Mwaka 2024, tani 522,788.33 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 4,352.7 zilivunwa ikilinganishwa na tani 479,976.62 zenye thamani ya bilioni 3,359.8 zilizovunwa mwaka 2023

**Kielelezo Na. 6.7. Mwenendo wa Uvunaji wa Samaki 2021 - 2024**




### Uuzaji wa Mazao ya Uvuvi na Samaki Nje ya Nchii

Mwaka 2024, samaki hai wa mapambo 173,377 na tani 59,746.41 za mazao ya uvuvi ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na samaki hai wa mapambo 166,024 na tani 42,371.41 za mazao ya uvuvi zilizouzwa mwaka 2023

## Kielelezo Na. 6.8 Mchanganuo wa Aina ya Uvunaji Samaki kwa Mwaka 2023



# VIWANDA

## Uzalishaji wa Bidhaa, Usajili, Ushindani na Udhibiti wa bidhaa bandia



### Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani

**4.9%**

Ongezeko la thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 26,438.5 mwaka 2023.



**Kielelezo Na. 7.1: Ukuaji wa Uzalishaji wa Baadhi ya Bidhaa za Viwandani Mwaka 2024**




Gharama za uzalishaji bidhaa viwandani zilikuwa wastani wa shilingi bilioni 12,236.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11,790.7 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Hii ilitokana na ongezeko la bei za baadhi ya malighafi zinazotumika katika uzalishaji viwandani zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.



**Kielelezo Na. 7.2: Uzalishaji wa Saruji, Mwaka 2020-2024**



## Usajili wa Viwanda na Biashara

**8.8%**

Ongezeko la kampuni zilizosajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA na kufikia kampuni 16,748 mwaka 2024 ikilinganishwa na kampuni 15,397 zilizosajiliwa mwaka 2023.

**4.4%**

Ongezeko la majina ya biashara yaliyosajiliwa na BRELA na kufikia 30,753 mwaka 2024 ikilinganishwa na majina ya biashara 29,448 mwaka 2023.

**10.4%**

Ongezeko la leseni za biashara daraja "A" zilitolewa na BRELA na kufikia 20,364 mwaka 2024 ikilinganishwa na leseni 18,448 zilizotolewa mwaka 2023.

**46.6%**

Ongezeko la leseni za viwanda zilizotolewa na BRELA mwaka 2024 ikilinganishwa na leseni 253 mwaka 2023.

Ongezeko la usajili na utoaji wa leseni lilitokana na uboreshwaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa leseni, na utoaji wa mafunzo kwa maafisa biashara na elimu kwa umma.

## Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo

**34.5%**

Ongezeko la sampuli zilizopimwa na kufikia 38724 mwaka 2024 ikilinganishwa na sampuli 28,791 zilizopimwa mwaka 2023.



Ongezeko la sampuli lilitokana na mwitikio wa wazalishaji na watumiaji wa bidhaa katika kuzingatia ubora na usalama wa bidhaa

## Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia

**3.7%**

Ongezeko la maombi ya muungano wa kampuni yaliyoidhinishwa na Tume ya Ushindani – FCC na kufikia maombi 56 mwaka 2024 ikilinganishwa maombi 54 mwaka 2023. Maombi hayo yalitoka katika sekta za kilimo, uzalishaji viwandani, fedha, afya, mawasiliano, madini, biashara na nishati.

Shilingi bilioni **17.9**

Thamani ya makasha 452 yenye bidhaa bandia kati ya makasha 6,357 yaliyokaguliwa na Tume ya Ushindani katika bandari ya Dar es Salaam na bandari kavu mwaka 2024. Bidhaa bandia zilizobainika zilikuwa za matumizi ya nyumbani, vifaa vya ujenzi, vipuri vya pikipiki na magari, shajala na vifaa vya kielektroniki.



# MADINI

## Leseni za Shughuli za Madini, Vibali, Madini



### Leseni za Shughuli za Madini

**6.7%**

Ongezeko la leseni za utafutaji wa madini, uchimbaji, uchenjuaji, usafishaji na biashara ya madini zilizotolewa na kufikia leseni 12,009 mwaka 2024.

**Hii ilitokana na juhudi za Serikali kuongeza vitendea kazi, kuboresha mfumo wa utoaji leseni na kutoa mafunzo kwa wa-tumiaji wa mfumo.**



## Vibali vya Uuzaji wa Madini

**4,176.18**

Dola za Marekani Milioni

Thamani ya vibali vya kuuza madini nje ya nchi kwa mwaka 2024, ambayo ni sawa na ongezeko la 20.1% ikilinganishwa na mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya madini ya dhahabu, makaa ya mawe na vito katika masoko ya nje ya nchi.

## Madini

### Dhahabu

**-5.3%**

Upungufu wa dhahabu zilizopata vibali vya kusafirishwa nje ya nchi na kufikia kilogramu 59,471.0 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na kilogramu 62,781.8 zilizopata vibali mwaka 2023. Hii ilitokana na Benki Kuu ya Tanzania kununua kilogramu 1,987.3 za dhahabu katika soko la ndani kwa lengo la kuimarisha akiba ya fedha za kigeni.

**Kielelezo Na. 8.1: Mwenendo wa Uzalishaji na Kiasi cha Dhahabu Kilichopata Vibali vya Kuuzwa Nje, Mwaka 2021 - 2024**




### Almasi

**220%**

Ongezeko la Thamani ya madini ya almasi yaliyozalishwa na kufikia karati 373,252.76 mwaka 2024 ikilinganishwa karati 132,636.2 na mwaka 2023.

### Vito vya Thamani

**-17.3%**

Upungufu wa madini ya vito ghafi (isipokuwa tanzanite na almasi) yaliyozalishwa na kufikia kilogramu 46,299,069 mwaka 2024, ikilinganishwa na kilogramu 55,954,779.72 zilizozalishwa mwaka 2023.

### Tanzanite

**-32.3%**

Upungufu madini ya tanzanite ghafi na magonga yaliyozalishwa na kufikia kilogramu 83,014.66 mwaka 2024 ikilinganishwa na kilogramu 122,664.95 zilizozalishwa mwaka 2023.

### Makaa ya Mawe

**19.9%**

Ongezeko la makaa ya mawe yaliyozalishwa na kufikia tani 3,904,542.69 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 3,256,481.06 zilizozalishwa mwaka 2023.



# NISHATI

## Uzalishaji wa Umeme, Gesi Asilia, Bei za Mafuta



### Uwezo wa Uzalishaji wa Umeme

**61.7%**

Ongezeko la uwezo wa uzalishaji wa umeme mwaka 2024 na kufikia megawati 3052.46 ikilinganishwa na megawati 1,887.5 mwaka 2023.

**Kielelezo Na 9.1: Ukuaji wa Uwezo wa Uzalishaji wa Umeme, Mwaka 2020-2024**




Mwaka 2024, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 11,958.84 ikilinganishwa na saa za gigawati 10,379.56 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 15.2.

**Kielelezo Na. 9.2: Mchanganuo wa Umeme Uliozalishwa Mwaka 2024**






**Kielelezo Na. 9.3: Mwenendo wa Mchango wa Umeme uliozalishwa katika Gridi ya Taifa kutoka Vyanzo Mbalimbali, Mwaka 2021-2024**




Mitambo ya nguvu ya maji iliongoza kwa kuchangia kiasi cha asilimia 51.9 cha umeme uliozalishwa katika Gridi ya Taifa kutokana na kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere.

# 10.7%

Ongezeko la umeme uliouzwa na kufikia saa za gigawati 9,114.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na saa za gigawati 8,232.0 zilizouzwa mwaka 2023.



**Kielelezo Na. 9.4: Umeme Uliouzwa kwa Watumiaji Mbalimbali, Mwaka 2020-2024**




## Gesi Asilia

# -18.4%

Upungufu wa uzalishaji wa gesi asilia mwaka 2024 hadi futi za ujazo milioni 69,538.3, ikilinganishwa na futi za ujazo milioni 85,173.2 zilizozalishwa mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 9.5: Mwenendo wa Uzalishaji wa Gesi Asilia, Mwaka 2020-2024**




**Kielelezo Na. 9.6: Mwenendo wa Bei ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa katika Soko la Ndani Mwaka 2024 (Shilingi/Lita)**






# 4 Miundombinu



# Mawasiliano
# Ujenzi
# Uchukuzi

# HABARI & MAWASILIANO

## Mawasiliano, Habari, Sanaa na Michezo



## Mawasiliano

### Huduma za Posta

**-31.2%**

Upungufu wa barua zilizosafirishwa na Shirika la Posta Tanzania na kufikia barua 789,299 mwaka 2024 ikilinganishwa na barua 1,146,627 mwaka 2023. Hii ilitokana na kukua kwa matumizi ya njia za kidigitali ka tika mawasiliano.



### Huduma za Simu

**23.6%**

Ongezeko la kadi za simu za kiganjani na kufikia 86,769,161 mwaka 2024 kutoka kadi 70,215,144 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 10.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Gharama za Kupiga Simu kwa Dakika, Mwaka 2021-2024**




### Huduma za Intaneti

**33.7%**

Ongezeko la kadi za simu zinazotumia intaneti na kufikia kadi milioni 48.0 mwaka 2024, ikilinganishwa na kadi za simu milioni 35.9 mwaka 2023.



**91.1%**

Ongezeko la matumizi ya intaneti nchini na kufikia Gigabaiti (GB) milioni 1,961 mwaka 2024 ikilinganishwa na Gigabaiti milioni 1,026 mwaka 2023.

## Habari



**61.1%**

Ongezeko la vituo vya redio vilivyosajiliwa na kupewa leseni na kufikia vituo 29 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kukua kwa hitaji la kupashana habari na kupungua kwa gharama za leseni kwa baadhi ya huduma kufuatia mabadiliko ya kanuni.



**Kielelezo Na. 10.2: Mchanganuo wa Usajili wa Vyombo vya Habari, Mwaka 2021 - 2024**




## Sanaa

**-8.9%**

Upungufu wa wasanii binafsi waliosajiliwa mwaka 2024 na kufikia wasanii binafsi 992 ikilinganishwa na wasanii 1,089 waliosajiliwa mwaka 2023.



**Kielelezo Na. 10.3: Mchanganuo wa Wasanii Binafsi Waliosajiliwa Mwaka 2024**




## Michezo



**13.5%**

Ongezeko la usajili wa wadau wa michezo na kufikia wadau 312 mwaka 2024, ikilinganishwa na wadau 275 mwaka 2023.



**Kielelezo Na. 10.4: Mwenendo wa Idadi Usajili wa Vilabu vya Michezo, Mwaka 2021-2024**



# UJENZI

## Mtandao wa Barabara, Usajili wa Makandarasi, Wahandisi



### Mtandao wa Barabara

**181,864.81**

Urefu wa mtandao wa barabara nchini kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na kilometa 181,655.49 mwaka 2023.



**Kielelezo Na.11.1: Usimamizi wa Mtandao wa Barabara**



**Kielelezo Na. 11.2: Hali ya Mtandao wwa barabara Kuu na za Mikoa**




**Kielelezo Na.11.3: Mchanganuo wa Wahandisi waliosajiliwa na Bodi ya Wahandisi kwa mwaka 2024**




## Usajili wa Makandarasi

**1,812**

Idadi ya makandarasi iliyosajiliwa na Bodi ya Makandarasi kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na makandarasi 1,807 mwaka 2023. Hii ilitokana uhamasishwaji uliofanywa na Bodi kuhusu uzingatiaji wa Sheria ya Usajili wa Makandarasi.

## Usajili wa Wahandisi

**22%**

Urefu wa mtandao wa barabara nchini kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na kilometa 181,655.49 mwaka 2023.Hii ilitokana na elimu iliyoendelea kutolewa kuhusu umuhimu wa usajili kwa wataalamu wa kada ya uhandisi.



# UCHUKUZI NA UHIFADHI MIZIGO

## Usafiri, Abiria na Shehena Zilizohudumiwa



### Usafiri

**Usafiri wa barabarani**

**10.3%**

Ongezeko la leseni zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini - LATRA kwa vyombo vilivyosajiliwa kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara na kufikia leseni 329,112 mwaka 2024 ikilinganishwa na leseni 298,270 zilizotolewa mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 12.1: Mwenendo wa Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, Mwaka 2021-2024**






**Ajali za barabarani**

**-6.8%**

Upungufu wa ajali zilizotokana na vyombo vya usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara na kufikia ajali 940 ikilinganishwa na ajali 1,009 mwaka 2023. Hii ilitokana na kaguzi za mara kwa mara barabarani, matumizi ya mfumo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi pamoja na elimu iliyotolewa kwa wadau wa vyombo vya usafiri barabarani. Sehemu kubwa ya ajali 40.7 ilihusisha bajaji/pikipiki

**Kielelezo Na. 12.2: Mchanganuo wa Ajali Mwaka 2024**



**Kielelezo Na. 12.3: Mwenendo wa Ajali za Barabarani, Mwaka 2020-2024**




## Abiria

### Usafiri wa Reli

Mwaka 2024, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania ilianza kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria kupitia reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa - SGR kati ya Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma kwa lengo la kurahisisha usafirishaji wa abiria na kuchochea shughuli za kiuchumi.

**1,395,119**

Abiria waliosafirishwa kupitia treni ya SGR katika mwaka 2024.

### Usafiri wa Anga

**8.1%**

Ongezeko la abiria waliosafiri kwa njia ya anga na kufikia 7,375,522 mwaka 2024, ikilinganishwa na abiria 6,820,541 mwaka 2023. Kati ya abiria waliosafirishwa mwaka 2024, abiria 1,164,210 walisafirishwa kupitia Shirika la ndege Tanzania(ATCL).




**Kielelezo Na. 12.4: Mchanganuo wa Abiria Mwaka 2024**




**17.9%**

Ongezeko la tani za mizigo zilisafirishwa mwaka 2024, ikilinganishwa na tani 36,265.0 zilizosafirishwa mwaka 2023. Kati ya tani zilizosafirishwa, tani 9,364 zilisafirishwa kwa kupitia Shirika la ndege Tanzania(ATCL).






## Shehena zilizohudumiwa

**10.2%**

Ongezeko la shehena zilizohudumiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA na kufikia tani milioni 29.05 mwaka 2024 ikilinganishwa na tanii milioni 26.36 zilizohudumiwa mwaka 2023.



**10.1%**

Ongezeko la shehena zilizohudumiwa katika Bandari Kuu za mwambao na kufikia tani milioni 28.15 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na tani milioni 25.56. Hii ilitokana na: Mamlaka kuendelea kuboresha miundombinu na huduma katika bandari na kujitangaza katika nchi za jirani; na kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi uliotokana na uwekezaji uliofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam.

**Kielelezo Na. 12.5: Mchanganuo wa Shehena Zilizohudumiwa kwa Bandari Mwaka 2024**








# 5
# Huduma za Jamii





Elimu
Afya
Maji

# ELIMU

## Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Elimu ya Ufundi Stadi-VETA, Elimu ya Juu



### Elimu ya Msingi

**Idadi ya Shule**

**4.1%**

Ongezeko la idadi ya shule za msingi na kufikia shule 20,533 mwaka 2024.



**Kielelezo Na. 13.1: Mwenendo wa Idadi ya Shule za Msingi Mwaka 2021-2024**




Ongezeko la idadi ya shule lilitokana na jitihada za Serikali kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule ya msingi.

**Kielelezo Na. 13.2: Mwenendo wa Idadi Shule za Msingi za Serikali na Zisizo za Serikali, Mwaka 2021-2024**




## Idadi ya Wanafunzi

**-0.3%**

Upungufu wa idadi ya wanafunzi katika shule za elimu ya msingi na kufikia 11,391,185 mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 11,425,482 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 13.3: Mgawanyo wa Wanafunzi kwa Jinsi katika Shule za Msingi Mwaka 2024**




**Kielelezo Na. 13.4: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na waliofaulu Darasa la Saba, Mwaka 2020-2024**




**Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi shule za Elimu ya Msingi za Serikali na zisizo za Serikali Mwaka 2024**

**1:50**

Uwiano huo ni zaidi ya kiwango cha 1:45 kinachokubalika kitaifa. Kutokana na hilo, Serikali inaendelea na juhudi za kuajiri walimu ili kuhakikisha uwiano sahihi wa mwalimu na wanafunzi.



## Elimu ya Sekondari

### Idadi ya Shule

**5.8%**

Ongezeko la Idadi ya shule za sekondari na kufikia 6,269 mwaka 2024 kutoka shule 5,926 mwaka 2023. Hii ilitokana na jitihada za Serikali za kuongeza idadi ya madarasa na shule mpya za sekondari pamoja na uwekezaji wa sekta binafsi.

**Kielelezo Na. 13.5: Mwenendo wa Idadi ya Shule za Sekondari, Mwaka 2021-2024**




**Kielelezo Na. 13.6: Mwenendo wa Idadi ya Shule za Sekondari za Serikali na Zisizo za Serikali, Mwaka 2021-2024**



# 7.7%

Ongezeko la idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita na kufikia wanafunzi 3,314,198 mwaka 2024, ikilinganishwa na wanafunzi 3,077,355 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 13.7: Mwenendo wa Idadi ya Wanafunzi Kidato cha I-VI, Mwaka 2021-2024**




**Kielelezo Na. 13.8: Mgawanyo wa Wanafunzi kwa Jinsia Katika Shule za Sekondari Kidato cha I-VI Mwaka 2024**




**Kielelezo Na. 13.9: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na Ufaulu Kidato cha Nne, Mwaka 2021-2024**






**Kielelezo Na. 13.10: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na Ufaulu Kidato cha Sita, Mwaka 2021-2024**




## Elimu ya Ufundi Stadi-VETA

# -22.7%

Upungufu wa idadi ya wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi – VETA mwaka 2023/24 na kufikia wanafunzi 30,728 ikilinganishwa na wanafunzi 39,764 mwaka 2022/23.





## Elimu ya Juu

### Idadi ya Wanafunzi

**6.4%**

Ongezeko la wanafunzi katika taasisi za elimu ya juu nchini na kufikia wanafunzi 334,854 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na wanafunzi 314,643 mwaka 2022/23. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa wanafunzi waliohitimu elimu ya sekondari na upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

**Kielelezo Na. 13.11. Mwenendo wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**




**Kielelezo Na. 13.12. Mchanganuo wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa Jinsia Mwaka 2023/24**




### Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Shilingi bilioni **738.2**

Thamani ya mikopo iliyotolewa na Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu mwaka 2023/24 ikilinganishwa na shilingi bilioni 635.7 mwaka 2022/23.



**13.7%**

Ongezeko la wanufaika wa Mikopo ya elimu ya juu iliyotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na kufikia 229,652 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na mwaka 2022/23.

**Kielelezo Na. 13.13: Mwenendo wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Wanufaika wa Mkopo Mwaka 2020/21-20023/24**



# AFYA

## Vituo vya Kutolea Huduma za Afya, Udhibiti wa Kifua Kikuu na Malaria, Afya kwa Watoto



### Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

**8.8%**

Ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya na kufikia vituo 12,846 mwaka 2024 ikilinganishwa na vituo 11,805 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 14.1: Mchanganuo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya kwa Umiliki Mwaka 2024**








**5.2%**

Ongezeko la wagonjwa waliohudumiwa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati na kufikia 47,495,667 mwaka 2024.



**6.2%**

Ongezeko la idadi ya wagonjwa waliolazwa katika na kufikia 1,866,106 ikilinganishwa na mwaka 2024.



**5.1%**

Ongezeko la idadi ya wagonjwa wa nje na kufikia 45,629,561 mwaka 2024.



**Kielelezo Na. 14.2: Mwenendo wa Idadi ya Wagonjwa Waliohudumiwa, Mwaka 2021-2024**




**Kielelezo Na. 14.3: Idadi ya Wagonjwa wa Nje katika Vituo vya vya kutolea Huduma za Afya, Mwaka 2021-2024**




**Kielelezo Na. 14.4: Idadi ya Wagonjwa Waliolazwa katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya, Mwaka 2021-2024**



## Udhibiti wa Kifua Kikuu

**-17.8%**

Kupungua kwa wagonjwa wa kifua kikuu na kufikia wagonjwa 76,684 mwaka 2024 ikilinganishwa na wagonjwa 93,184 mwaka 2023.

**4.9%**

Ongezeko la idadi ya vituo vya uchunguzi na tiba ya kifua kikuu na kufikia 1,859 mwaka 2024 ikilinganishwa na vituo 1,773 mwaka 2023.

## Udhibiti wa Malaria

Mwaka 2024, vipimo 9,644,925 vya malaria na vichupa 3,739,685 vya dawa ya sindano ya kutibu malaria kali vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya afya.

**Kielelezo Na. 14.5: Mwenendo wa Ununuzi wa Dawa, Vyandarua na Vitendanishi, Mwaka 2023-2024**




## Afya kwa Watoto

**5.4%**

Ongezeko la idadi ya watoto waliozaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya na kufikia watoto 2,219,417 Mwaka 2024.





**Kielelezo Na. 14.6: Watoto wa Chini ya Mwaka Mmoja Waliopata Chanjo Mwaka 2024**





# MAJI

## Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji, Upatikanaji wa Maji, Uondoaji wa Majitaka



### Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

Mwaka 2024, kiwango cha rasilimali za maji kinachofaa kwa matumizi kilikuwa wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka kama kilivyokuwa mwaka 2023.

**2,105**

Mita za Ujazo

Kiasi cha maji kwa mtu ambacho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.



**Kielelezo Na. 15.1: Mchango wa Mapato ya Mamlaka za Maji kwa Mwaka 2024**



## Upatikanaji wa Maji

**Kielelezo Na. 15.2: Mwenendo wa Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji Mijini na Vijijini, Mwaka 2021-2024**




## Uondoaji wa Majitaka

**Kielelezo Na. 15.3: Wateja walioonganishwa na mtandao wa majitaka, Mwaka 2021-2024**




**Kielelezo Na. 15.4: Mtandao wa majitaka, Mwaka 2021-2024**






**Kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa maji kulitokana na Serikali kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya maji mijini na vijinini**



# 6 Sekta Nyingine



Utalii
Sekta Binafsi
Masuala mtambuka

# MALIASILI NA UTALII

## Utalii & Hifadhi za Taifa



### Utalii

**18.5%**

Ongezeko la watalii walioingia nchini na kufikia watalii 2,141,895 mwaka 2024 ikilinganishwa na watalii 1,808,205 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuendelea kutangaza utalii kupitia: programu maalumu (The Royal Tour na Amazing Tanzania); balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali; na matamasha na mikutano.




**15.7%**

Ongezeko la mwaka la thamani ya mapato ya utalii na kufikia dola za Marekani milioni 3,903 mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 16.1: Mwenendo wa Biashara ya Utalii Nchini, Mwaka 2021-2024**




**Kielelezo Na. 16.2: Mchanganuo wa Watalii Waliongia Nchini kwa Maeneo Waliotembelea Mwaka 2024**






## Hifadhi za Taifa

**Kielelezo Na. 16.3: Mchanganuo wa Watalii waliotembelea Hifadhi za Taifa 2024**




Mwaka 2024, Watalii 2,010,239 walitembelea Hifadhi za Taifa ikilinganishwa na watalii 1,790,682 mwaka 2023.

# UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

## Usajili wa Miradi ya Uwekezaji & Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje



### Usajili wa Miradi ya Uwekezaji

**71.3%**

Ongezeko la miradi iliyosajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania - TIC mwaka 2024. Fursa za ajira kutokana na miradi hiyo ziliongezeka na kufikia 212,293 mwaka 2024 ikilinganishwa na ajira 137,010 mwaka 2023.

**62.8%**

Ongezeko la thamani ya miradi iliyosajiliwa na kufikia dola za Marekani milioni 9312.69 mwaka 2024 kilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,720.4 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 17.1: Mchanganuo wa Miradi iliyosajiliwa Mwaka 2024**




### Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje

**3.9%**

Ongezeko la uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje na kufikia dola za Marekani milioni 23,042.5 mwaka 2023 kutoka dola za Marekani milioni 22,182.41 mwaka 2022.

**19,139.6**

Dola za Marekani milioni

Thamani ya uwekezaji wa moja kwa moja kwa mwaka 2023 kutoka dola za Marekani 18,095.8 mwaka 2022.

## Kielelezo Na. 17.2: Mchanganuo wa Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje ya Nchi Mwaka 2023






# MASUALA MTAMBUKA

## Mazingira, Usalama wa Raia, pamoja na Usajili, Ufilisi na Udhamini



### Mazingira

**40.0%**

Ongezeko la miradi iliyopata hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kufikia miradi 1,764 mwaka 2024 ikilinganishwa na miradi 1,260 mwaka 2023.

**7.4%**

Ongezeko la miti iliyopandwa na kufikia miti 286,657,203 mwaka 2024 ikilinganishwa na miti 266,970,203 mwaka 2023.



### Usalama wa Raia

**5.7%**

Upungufu wa makosa makubwa ya jinai yalitolewa taarifa na wananchi na kufikia makosa 50,574 mwaka 2024 ikilinganishwa na makosa 53,640 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 18.1: Mchanganuo wa Makosa Makubwa ya Jinai Mwaka 2024**




### Usajili, Ufilisi na Udhamini

**81.2%**

Ogezeko la hati za talaka zilizosajiliwa na kufikia hati 1,569 mwaka 2024, ikilinganishwa na hati za talaka 866 zilizosajiliwa mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 18.2: Mwenendo wa Hati za Viapo vya Ndoa na Hati za Talaka, Mwaka 2021-2024**



**Kielelezo Na. 18.3: Idadi ya Usajili wa Hati Mbalimbali chini ya Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA kwa Mwaka 2024**





# 7

# Suala Maalumu



# Uendelezaji wa Nishati Safi ya Kupikia

# UENDELEZAJI WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

Utangulizi, Hali Ilivyo, Athari za Matumizi ya Nishati Isiyo Safi ya Kupikia Changamoto Zinazoathiri Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, Mpango wa Serikali



## Utangulizi

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Benki ya Dunia (2020) na Shirika la Afya Duniani (2021), **nishati safi ya kupikia hupimwa kwa vigezo kama vile ufanisi, usalama, upatikanaji, unafuu wa gharama, na utoaji chembechembe ndogo** za vumbi zenye ukubwa usiozidi 2.5µm (PM2.5)



Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024–2034) unaeleza kuwa nishati safi ni ile inayotoa moshi kidogo na inalenga kuboresha afya, mazingira, na maisha ya wananchi, huku ikisaidia kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya kupunguza mabadiliko ya tabianchi.

### Lengo

i. Kuhakikisha uwepo wa usalama, uendelevu na urahisi wa upatikanaji wa nishati ya kupikia, kuokoa muda, kupunguza gharama za matumizi pamoja na athari za kimazingira na kiafya kwa watumiaji.

ii. Kutekeleza makubaliano ya kitaifa na kimataifa yanayolenga kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uzalishaji wa gesi joto (greenhouse gas) duniani.

### Sera na Mikakati ya Kitaifa Inayohusiana na Nishati Safi ya Kupikia

Serikali imeanzisha sera na mikakati kadhaa ili kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi, ikiwemo:

Sera ya Nishati (2015): Kuboresha maisha kupitia nishati za kisasa.

Sera ya Mazingira (2021): Kuhifadhi misitu kwa kutumia nishati mbadala.

Sera ya Misitu (1998): Usimamizi endelevu wa misitu.

Sera ya Afya (2007): Kulinda mazingira kwa faida ya afya ya jamii.

Sera ya Maendeleo ya Mwanamke na Jinsia (2000): Kupunguza mzigo wa wanawake katika kutafuta kuni na maji.

## Hali Ilivyo

**39,023.94**

Uzalishaji wa hewa ukaa (carbon dioxide emission) duniani mwaka 2023 kutoka kutoka tani milioni 25,725.44 mwaka 2000.

**Kielelezo Na. 19.1: Uzalishaji wa Hewa Ukaa Kikanda**






China, Marekani na India zinaongoza kwa uzalishaji mkubwa wa hewa ukaa.

Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki – EAC, Kenya iliongoza Tanzania ni ya pili kwa uzalishaji wa hewa ukaa ambapo tani milioni 19.37 zilizalishwa mwaka 2023 ikilinganishwa na tani milioni 3.11 mwaka 2000.

**Kielelezo Na. 19.2:Uzalishaji wa Hewa Ukaa katika Ngazi ya Nchi Mwaka 2000 na 2023**




### Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Duniani

Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara zina kiwango kidogo cha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ambacho hakiendani na ongezeko la idadi ya watu ikilinganishwa na nchi za Asia, hususan Asia Mashariki na Kusini pamoja na nchi za Latini Amerika na Caribbean ambazo zina mwenendo mzuri wa upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia.

**Kielelezo Na. 19.3: Upatikanaji wa Nishati Safi na Teknolojia ya Kupikia Kikanda Mwaka 2000 na 2022 (Asilimia)**




### Matumizi ya Nishati Safi Tanzania



**9.20%**

Ongezeko la idadi ya watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia kwa mwaka 2024 kwa mujibu wa benki ya Dunia. Kiwango hiki ni chini ya kiwango cha wastani cha dunia cha asilimia 73.74 na cha nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara cha asilimia 22.24 kwa mwaka 2022

**Kielelezo Na. 19.4: Mwenendo wa Matumizi ya Nishati Safi na Teknolojia ya Kupikia Tanzania Mwaka 2010 – 2022**



Kwa mujibu wa Mpangokazi wa Nishati ya Kupikia wa Mwaka 2022, asilimia 82 ya nishati kuu inayotumika nchini inatokana na tungamotaka (biomass).

**Kielelezo Na. 19.5: Matumizi ya Nishati ya Kupikia kwa Kaya, 2019/20**




### Hali Ilivyo ya Nishati na Teknolojia za Kupikia Nchini



Serikali ya Tanzania imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya upatikanaji wa nishati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na umeme, gesi asilia, bayogesi, bayoethano, na gesi ya mitungi (LPG). Hali ya matumizi ya nishati ya kuni na mkaa bado ni ya juu, hasa vijijini na mijini mtawalia, ingawa imepungua kidogo kutokana na jitihada za serikali za kuhamasisha matumizi ya nishati safi.

**Kielelezo Na. 19.6: Matumizi ya Kuni Kama Nishati ya Kupikia katika Ngazi ya Mkoa, Mwaka 2017/18 (Asilimia ya Kaya)**




**Kielelezo Na. 19.7: Matumizi ya Mkaa Kama Nishati ya Kupikia katika Ngazi ya Mkoa Mwaka 2017/18 (Asilimia ya Kaya)**




**Kielelezo Na. 19.8: Mwenendo wa Matumizi wa Nishati ya Kuni na Mkaa Mwaka 2007 – 2017/18 (Asilimia ya Kaya)**




Umeme unazidi kuenea nchini kupitia miradi ya serikali, lakini bado kuna tofauti kubwa ya upatikanaji kati ya mijini (asilimia 73.2) na vijijini (asilimia 24.5). Nishati nyingine kama kinyesi cha wanyama, mabaki ya mimea na mafuta ya taa bado zinatumika kwa kiasi kidogo, huku changamoto zake zikiwemo gharama, athari za kiafya na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mbadala wa nishati hizo.



Kwa ujumla, mafanikio ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi nchini yanategemea juhudi zaidi za kuboresha miundombinu, kutoa ruzuku, kuongeza uelewa wa jamii na kutatua changamoto za kiuchumi na kiteknolojia zinazokwamisha upatikanaji wa nishati mbadala kwa wananchi wote.

## Athari za Matumizi ya Nishati Isiyo Safi ya Kupikia

**i. Athari za Kiafya:**

Moshi wa nishati isiyo safi husababisha magonjwa ya mfumo wa upumuaji kama vile pumu, kifua kikuu, na saratani ya mapafu. Huweza pia kusababisha matatizo ya ujauzito na magonjwa ya moyo, macho, na kupooza. Ubebaji wa kuni husababisha maumivu ya mgongo, na huchangia vifo zaidi ya 33,000 kwa mwaka nchini.



**ii. Athari za Kimazingira:**

Matumizi ya nishati isiyo safi huchangia uharibifu wa mazingira. Gesi chafu kama kaboni huongeza mabadiliko ya tabianchi na maafa kama ukame, mafuriko na kuyeyuka kwa barafu. Hii husababisha pia upotevu wa viumbehai na kuongezeka kwa chumvi baharini.



**iii. Ukataji hovyo wa misitu:**

Kiasi cha hekta 469,420 za misitu hukatwa kila mwaka kwa kuni na mkaa. Hali hii husababisha ukame na madhara ya kiikolojia. Tayari asilimia 16 ya nchi imegeuka kuwa jangwa kutokana na ukataji wa miti



**iv. Athari za Kijamii:**

Wanawake na watoto hukumbana na ukatili wa kijinsia na hatari nyingine wakiwa katika harakati za kutafuta kuni. Wanawake pia hupigwa kwa kuchelewa kurudi nyumbani, na hukosa kushiriki shughuli za kijamii na kiuchumi

Matumizi ya nishati chafu husababisha macho mekundu na kuhusishwa na imani za kishirikina.



**v. Athari za Kiuchumi:**

Kutafuta kuni huchukua takribani saa sita kwa siku, kupunguza muda wa kufanya kazi za maendeleo. Hii hupunguza nafasi za kuongeza kipato au kujiendeleza kielimu




**vi. Athari za Kielimu:**

Watoto wanaoshiriki kutafuta kuni hukosa muda wa masomo na hushuka kitaaluma. Wanawake pia hukosa fursa za kujielimisha kutokana na shughuli hizi.



## Changamoto Zinazoathiri Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia



i. Uelewa mdogo wa wananchi na taasisi kuhusu madhara ya nishati isiyo safi unachelewesha mabadiliko kuelekea matumizi ya nishati safi ya kupikia.

ii. Upatikanaji hafifu wa nishati safi, nafuu na ya uhakika unakwamisha uhamaji wa wananchi kuelekea matumizi yake.

iii. Gharama kubwa za vifaa, majiko na matumizi ya nishati safi huwazuia wananchi wengi kumudu kuvitumia.

iv. Kutokuwiana kwa sera na sheria mbalimbali kunapingana na juhudi za kuendeleza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

v. Uwekezaji mdogo na uhamasishaji hafifu kwa wadau huzuia maendeleo ya mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia.

vi. Taasisi nyingi hazina uwezo wa kutosha kifedha, kiujuzi na katika rasilimali watu wa kutekeleza miradi ya nishati safi.

vii. Ukosefu wa tafiti, ubunifu na teknolojia husababisha ukosefu wa takwimu sahihi, ongezeko la gharama na mipango duni ya kukuza nishati safi ya kupikia.

## Mpango wa Serikali

Kutokana na athari mbaya za kiafya, kimazingira na kiuchumi zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia kama mkaa na kuni, matumizi ya nishati safi yanaonekana kuwa suluhisho muhimu. Nishati safi husaidia kuboresha afya ya jamii, kulinda mazingira na kuimarisha uchumi wa kaya na taifa kwa ujumla. Hata hivyo, changamoto kama ukosefu wa miundombinu, uelewa mdogo kuhusu faida za nishati safi, na hali ngumu ya kifedha kwa kaya maskini, zinakwamisha matumizi yake.

Serikali tayari imeandaa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034), unaolenga kuwahusisha wadau wote katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi, hasa kwa wanawake ambao huathirika zaidi na matumizi ya nishati chafu. Lengo kuu la mkakati huu ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2034, asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia, ikilinganishwa na asilimia 9.2 mwaka 2022.






Matumizi ya Nishati ya Kupikia kwa Kaya Tanzania Bara 2019/20






Wizara ya Fedha
Mji wa serikali-Mtumba
Mtaa wa hazina
S.L.P 2802
Dodoma
https://www.mof.go.tz